**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 21/12/2021.**

**Mahudhurio**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mh. Bahati Henerico | Mwenyekiti |
| 2. | Mh. Clarence Rugimbana | Mjumbe |
| 3. | Mh. Beneth Byarufu | Mjumbe |
| 4. | Mh. Kashunju Runyogote | Mjumbe |
| 5. | Mh. Jonas Vedasto | Mjumbe |
| 6. | Mh. Chrisant Callist | Mjumbe |
| 7. | Mh. Ngalinda A.Marick | Mjumbe |
| 8. | Mh. Mary K.Katabaro | Mjumbe |
| 9. | Mh. Adorophina Katonya | Mjumbe |
| 10 | SACF James M. John | Katibu |

Wasiohudhuria

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Innocent Bilakwate (Mbunge) | Kwa taarifa |

**Wataalam**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Revocatus Josephat | Mkuu wa Idara ya maendeleo ya jamii, vijana na ustawi wa jamii |
| 2. | Ndg. Henerico Rushala | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 3. | Ndg. M. Z. Mtafungwa | Kny: Katibu Tawala wa Wilaya |
| 4. | Ndg. Zaveria Mpoli | Kny: Mkaguzi wa ndani |
| 5. | Eng. Yesse N.Yesse | Kaimu Mkuu wa Idara ujenzi na zimamoto |
| 6. | Ndg. Evarista Chacky | Kny Mratibu wa kitengo cha nyuki |
| 7. | Ndg. Alexander Lundera | Afisa TEHAMAU |
| 8. | Ndg. Meshack Libent | Mkuu wa Idara ya kilimo, ushrika na umwagiliaji |
| 9. | Ndg. Damian Barabona | Mdhibiti ubora wa Elimu Wilaya |
| 10. | Dr. Diocles Ngaiza | Mganga Mkuu wa Wilaya |
| 11. | Ndg. Richard Mayiku | Kaimu mkuu wa Idara ya ardhi na maliasili |
| 12. | Ndg. Prosper Rutakinikwa | Kaimu mkuu wa Idara ya mifugo na uvuvi |
| 13. | CPA Alfred N. Irangi | Kaimu Mkuu wa Idara ya fedha na biashara |
| 14. | Ndg. Ramadhan Y.Marwa | Mkuu wa Idara ya Elimu msingi |
| 15. | Ndg. Zephrine Kabona | Katibu TSC |
| 16. | Ndg. Mayala P. Sengerema | Afisa uchaguzi |
| 17. | Ndg. Yasin Mwinory | Kaimu mkuu wa Idara ya mazingira na taka ngumu |

**Sekretarieti**

1. Golden Nzalalila



Scanned with CamScanner

**Agenda**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha dondoo
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 26/11/2021
4. Utekelezaji wa maazimio kikao kilichopita cha tarehe 26/11/2021
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Julai hadi Novemba 2021/2022
6. Mabadiliko ya ramani ya jengo la Halmashauri
7. Kufunga kikao

**KU/KYR/KFUM/20/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kueleza kuwa ni kikao cha kawaida kujadili taarifa ya mapato na matumizi mwezi Novemba 2021. Baada ya kusema hayo alifungua kikao mnamo saa 11:45 asubuhi

**KU/KYR/KFUM/21/2021/2022 KUTHIBITISHA DONDOO**

Dondoo zilithibitishwa na kuongeza agenda ya 'kubadilisha ramani ya jengo la Halmashauri' na kuwa agenda namba 06.

**KU/KYR/KFUM/22/2021/2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 26/11/2021**

Muhtasari ulisomwa haukuwa na masahihisho hivyo ulisainiwa na kuwa kumbukumbu halali.

**KU/KYR/KFUM/23/2021/2022 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 26/11/2021.**

**Hoja:** Vifuatiliwe vikundi 4 ambavyo havikufika kuchukua fedha wakati Mkuu wa Wilaya anawapa hundi vikundi vya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

Utekelezaji: Vikundi Goodhope (Isingiro) waliopangiwa kukopeshwa Tsh. 6,000,000/=, Abakazi Tweyambe (Nkwenda) Tsh. 5,000,000/=, Mwanzo (Nyakatuntu) Tsh. 6,140,000/= na Ushindi (Kaisho) Tsh. 4,000,000/= waliitwa ofisini tarehe 29/11/2021 na waliweza kukamilisha utaratibu na kujaza mikataba na utaratibu wa malipo ya mikopo yao unaendelea.

Mjumbe alihoji kuwa vikundi vyote viliweza kufika kwa Mkuu wa Wilaya?

Ufafanuzi: vikundi vyote vilifika kwa Mkuu wa Wilaya.

Ilihojiwa kuwa ni sababu gani iliyosababisha vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu washindwe kufika kwa Mkuu wa Wilaya?

Jibu, Hawakupata taarifa kwa wakati kutoka kwa Watendaji wa kata.



Scanned with CamScanner

Hoja: Afuatiliwe ndg. Godwine Mwijage katika mwenendo wake wa kazi ili aweze kuchukuliwa hatua.

Utekelezaji: Amefuatiliwa na kukuta mwenendo wake kazi siyo mzuri hivyo mkataba wake wa kazi umesitishwa tangu tarehe 14/12/2021 na kuweka mkusanyaji mwingine wa mapato ya stendi.

**KU/KYR/KFUM/24/2021/2022 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2021 (2021/2022)**

**Makisio ya mapato na matumizi**

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 imekisia kukusanya na kutumia kiasi cha Tsh**. 33,638,704,700.64**. Fedha hizi zinatokana na vyanzo mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Mapato ya ndani (vyanzo visivyofungiwa na vyanzo fungiwa) Tsh. 2,653,439,345.00
- Ruzuku ya Mapato mengineyo - other charges grants (O.C) Tsh. 1,574,396,000.00
- Mishahara Tsh. 16,824,185,000.00
- Fedha za maendeleo kutoka Serikali kuu Tsh.5,842,093,815.64
- Fedha za maendeleo kutoka kwa wafadhili/ wahisani Tsh.5,722,481,464.00
- Michango ya jamii Tsh. 605,000,000.00

**Mapokezi**

Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imekusanya na kupokea kiasi cha Tsh. **13,573,094,909.64** ambayo ni sawa na asilimia **40.35** ya lengo la mwaka.

- Mapato ya ndani (vyanzo visivyofungiwa) Tsh.1,510,141,336.68 sawa na asilimia 75.55
- Mapato ya ndani (vyanzo fungiwa) Tsh.203,260,000.33 sawa na asilimia 31.05
- Ruzuku ya Mapato mengineyo - other charges grants (O.C) Tsh. 1,122,970,4541.47 sawa na asilimia 71.33.
- Mishahara Tsh. 7,6101,012,760.00 sawa na asilimia 42.21
- Fedha za maendeleo kutoka Serikali kuu Tsh. 900,017,478.45 sawa na asilimia 15.08
- Fedha za maendeleo kutoka kwa wafadhili/wahisani Tsh.170,856,970.20 sawa na asilimia 2.84
- Michango ya jamii Tsh.254,950,000.00 sawa na asilimia 42.14.
- Zimepokelewa fedha zilizotolewa nje ya bajeti (COVID 19) Tsh. 2,309,885,822.51kwa mchanaganuo ufuataO:-



Scanned with CamScanner

- Ujenzi wa vyumba vya madarasa themanini na tano (85) Idara ya elimu sekondari Tsh. 1,700,000,000
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa Ishirini na nne (24) Idara ya elimu msingi Tsh. 480,000,000
- Ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1) kituo cha Afya Murongo Tsh.90,000,000
- Uhamasishaji wa chanjo ya uviko 19 Tsh. 33,371,075.51
- Ufuatiliaji na tathmini Tsh. 6.514,746

**Matumizi**

Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imekusanya na kutumia kiasi cha Tsh. **12,523,416,489.73** ambayo ni sawa na asilimia **37.23** ya lengo la mwaka.

- Matumizi ya kawaida vyanzo vya ndani (60%) Tsh.327,774,767.65 sawa na asilimia 27.33
- Matumizi ya Ruzuku ya Mapato mengineyo - other charges grants (O.C) Tsh. 816,124,110.00 sawa na asilimia 51.84
- Matumizi ya ruzuku ya Mishahara Tsh. 7,101,012,760.00 sawa na asilimia 42.21
- Matumizi fedha za maendeleo kutoka mapato ya ndani (40%) Tsh. 616,317,491.64 sawa na asilimia 77.08
- Matumizi fedha za maendeleo kutoka Serikali kuu Tsh. 695,819,729.18 sawa na asilimia 76.85
- Matumizi fedha za maendeleo kutoka kwa wafadhili/wahisani Tsh.198,271,808.75 sawa na asilimia 3.30
- Matumizi fedha za mapato fungiwa Tsh. 203,260,000.00 sawa na asilimia 31.05
- Matumizi ya fedha za michango ya jamii Tsh.254,950,000.00 sawa na asilimia 42.14
- Matumizi ya fedha zilizopokelewa nje ya bajeti (COVID 19) Tsh. 2,309,885,822.51kwa mchanaganuo ufuatao:-


- Ujenzi wa vyumba vya madarasa themanini na tano (85) Idara ya elimu sekondari Tsh. 1,700,000,000
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa Ishirini na nne (24) Idara ya elimu msingi Tsh. 480,000,000
- Ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1) kituo cha Afya Murongo Tsh.90,000,000
- Uhamasishaji wa chanjo ya uviko 19 Tsh. 33,371,075.51
- Ufuatiliaji na tathmini Tsh. 6.514,746


Baada ta taarifa kuwasilishwa wajumbe walihoji na kushauri kama ifuatavyo:-

Hoja: Kipengele cha mapato ya ndani maendeleo na mfuko wa WWU hakina fedha kutoka mapato ya ndani.



Scanned with CamScanner

Majibu: Vipengele hivyo vimeshapokea fedha kwa zaidi ya 60% (zaidi ya malengo) na mwezi huu kulikuwa na mambo mengi hivyo zilitumika kwenye kifungu cha matumizi ya kawaida (recumbent) kwa kiasi kikubwa.

Mjumbe aliwashukuru wataalam kwa usimamizi wa fedha za uviko 19 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuomba kupewa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Ufafanuzi: Ujenzi unaendelea na upo hatua za mwisho na mpaka kufikia leo tarehe 21/12/2021 ujenzi umefikia 98% na utakamilika mapema na wanafunzi wataanza kutumia vyumba hivyo kuanzia Januari 2022.

**KU/KYR/KFUM/25/2021/2022 MABADILIKO YA RAMANI YA JENGO HALMASHAURI**

Limewasilishwa ombi la kupata ukumbi wa mikutano kwenye jengo la utawala linaloendelea kujengwa baada ya Mhadisi Mshauri kufanya usanifu upya kwenye gorofa ya juu. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ni uhitaji wa ukumbi huo ili kuweza kupunguza gharama za kukodi ukumbi.

Wajumbe baada ya kusoma ramani walipongeza kwa kufanya jambo hilo kwa kuwa itapunguza gharama kwa Halmashauri za kukodi kumbi, hivyo kikao kiliridhia suala hili kwa kuwa hakuna ongezeko la gharama na ni tija kwa Halmashauri.

**KU/KYR/KFUM/26/2021/2022 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na kuwashukuru kwa ushirikiano wanaotoa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo mbalimbali. Baada ya kusema hayo alifunga kikao mnamo saa 7:00 mchana.

Saini............................ Saini............................

Jina M.P.SENGEREMA Jina Bahati Henerico

Katibu Mwenyekiti

Tarehe 09/02/2022.



Scanned with CamScanner